# Serikali Mtandao

www.ega.go.tz

Jarida toleo la 16 : Aprili - Juni 2026



# Serikali yazindua Mifumo ya GSD na Ngao



Serikali yawatuku tunzo walioshiriki kutengeneza Mifumo ya GSD na Ngao

Serikali yazindua Mifumo ya GSD na NGAO Kuimarisha Huduma za Umma >>>Uk. 01

Naibu Waziri - UTUMISHI Ahamasisha Ubunifu wa Teknolojia Zinazochipukia Kuboresha Huduma Serikali >>>Uk. 07

Epuka Dawa za Miujiza, Chagua Njia Salama ya Kupunguza Uzito >>>Uk. 12

TEHAMA ilivyobadili Maisha ya Joseph kutoka Utegemezi hadi Ubunifu >>>Uk. 16

# Yaliyomo


| Kichwa | Ukurasa |
| --- | --- |
| Nukuu ya Mwenyekiti wa Bodi | iii |
| Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu | iv |
| Tahariri | v |
| **Habari** Serikali yazindua Mifumo ya GSD na NGAO Kuimarisha Huduma za Umma | 1 |
| **Habari** Waziri Kikwete: Serikali Mtandao yazidi Kuimarika | 3 |
| **Habari** Bi. Khadija Mzenzi Tuzo ya Mfanyakazi Bora e-GA 2025/2026 | 5 |
| **Habari** Naibu Waziri - UTUMISHI ahamasisha Ubunifu wa Teknolojia Zinazochipukia Kuboresha Huduma za Serikali | 7 |
| **Habari** Mhe. Ridhiwani Aipongeza e-GA Ujenzi wa Mifumo Bunifu | 10 |
| **Makala** Epuka Dawa za Miujiza, Chagua Njia Salama ya Kupunguza Uzito | 12 |
| **Vijana ana TEHAMA** TEHAMA Ilivyobadili Maisha ya Joseph kutoka Utegemezi hadi Ubunifu | 16 |
| **Mfumo wa leo** e-Ardhi : Mageuzi ya Kidijiti yanavyosogeza Huduma za Ardhi Karibu na Wananchi | 20 |
| Matukio katika picha | 22 |



## Bodi ya Wahariri

| | |
| --- | --- |
| **Mwenyekiti** | Eng. Benedict B. Ndomba<br>Mkurugenzi Mkuu |
| **Mhariri** | Subira J. Kaswaga<br>Meneja Habari na Mawasiliano |
| **Wajumbe** | SACP. Hamis Ali<br>Mkaguzi Mkuu wa ndani<br>SACP. Rafael Ruthahiwa<br>Meneja Huduma za Sheria<br>Long'ida Oltetiai<br>Meneja Huduma kwa wateja na Takwimu |
| **Wapiga picha** | Benchine Bago<br>Afisa Habari<br>Mussa Enock<br>Afisa Habari |
| **Msanifu** | Edger Msamba<br>Afisa TEHAMA |



"

**Mfumo wa NGAO unaweka msingi wa Serikali salama kidijitali kwa kutumia uthibitishaji wa vipengele vingi (Multi-Factor Authentication), hatua muhimu katika kukabiliana na hatari za kimtandao. Sambamba na ujenzi wa mfumo huo, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itaendelea kuwajengea uwezo watumiaji wa mifumo ya Serikali kuhusu matumizi salama ya TEHAMA na mbinu za kujikinga dhidi ya matishio ya kimtandao, ili kuimarisha usalama wa taarifa na kuhakikisha huduma za Serikali zinaendelea kutolewa kwa ufanisi na kwa usalama.**

"

Dkt. Mussa Kissaka
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi - e-GA

# Umuhimu wa Kuwasilisha andiko la Mradi wa TEHAMA Kupitia GISP



Mageuzi ya kidijitali yanayoendelea Serikalini yanahitaji uwekezaji wa kimkakati katika miradi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambayo inaleta matokeo chanya kwa wananchi na Serikali kwa ujumla. Ili kufanikisha azma hiyo, ni muhimu kila taasisi ya umma ihakikishe kuwa miradi yake ya TEHAMA inapangwa, inapitiwa na kutekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao.

Katika kutimiza jukumu hilo, matumizi ya Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini 'Government ICT Service Portal - (GISP) yamekuwa nyenzo muhimu ya kuratibu uwasilishaji, tathmini na uidhinishaji wa maandiko ya miradi ya TEHAMA ya taasisi za umma. Mfumo huu umeanzishwa ili kuhakikisha uwekezaji wa Serikali katika TEHAMA unafanyika kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia matumizi bora ya rasilimali za umma.

Kuwasilisha andiko la mradi kupitia GISP si hitaji la kiutaratibu pekee, bali ni hatua muhimu inayowezesha kuhakikisha mradi wa TEHAMA unaendana na Sheria, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao. Vilevile, mfumo huu husaidia kubaini fursa za kutumia mifumo shirikishi na miundombinu ya pamoja iliyopo serikalini, hivyo kupunguza urudufu wa uwekezaji na kuongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aidha, mapitio ya kitaalamu yanayofanyika kupitia GISP huchangia kuongeza ubora wa miradi ya TEHAMA kwa kutathmini uhalali wake wa kiufundi (technical part), kiusalama, kifedha na kiutendaji kabla ya utekelezaji. Hali hii huongeza thamani ya fedha za umma na kuhakikisha mifumo inayojengwa inaweza kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali na inakuwa endelevu.

Tunapojenga Serikali Mtandao, tunapaswa kutambua kuwa mafanikio ya kila mradi wa TEHAMA yanategemea uwezo wake wa kubadilishana taarifa na mifumo mingine, kuzingatia viwango vya usalama wa taarifa na kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya wananchi pamoja na yale ya taasisi husika. Hivyo, GISP ni chombo muhimu kinachowezesha kufikiwa kwa malengo hayo kwa kuhakikisha miradi yote ya TEHAMA inaratibiwa kwa mtazamo wa kitaifa.

Ninatoa wito kwa viongozi wa taasisi zote za umma kuhakikisha kuwa kila andiko dhana la mradi wa TEHAMA linawasilishwa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kupitia GISP katika hatua za awali za maandalizi. Ushirikiano huu utasaidia kujenga mazingira ya uwekezaji wenye tija, kuimarisha uratibu wa miradi ya TEHAMA na kuharakisha utekelezaji wa ajenda ya mageuzi ya kidijitali katika utendaji wa Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa pamoja, tunaweza kuhakikisha kuwa kila mradi wa TEHAMA unakuwa sehemu ya suluhisho la kujenga Serikali Mtandao iliyo salama, jumuishi, inayounganishwa na inayotoa huduma bora kwa wananchi wote.

# Ushirikiano wa Taasisi : Msingi wa Ujenzi wa Serikali Mtandao Imara na Jumuishi



**Bi. Subira Kaswaga**
**Meneja Mawasiliano e-GA**

Mageuzi ya kidijitali yanaendelea kubadilisha namna serikali duniani zinavyopanga, kusimamia na kutoa huduma kwa wananchi. Tanzania nayo imeendelea kupiga hatua katika kujenga Serikali Mtandao inayolenga kuboresha utoaji wa huduma za umma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Hata hivyo, mafanikio ya safari hii hayategemei uwekezaji katika teknolojia pekee, bali yanategemea kwa kiwango kikubwa ushirikiano wa taasisi za umma katika kupanga, kutekeleza na kuendesha mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini.

Dhana ya Serikali Mtandao imejengwa katika matumizi ya TEHAMA yanayolenga kuboresha utendaji wa serikali, kuongeza uwazi na uwajibikaji, kuharakisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuchochea maendeleo ya uchumi wa kidijitali. Ili kufikia malengo haya, ni lazima mifumo na miundombinu ya taasisi mbalimbali iweze kuwasiliana, kubadilishana taarifa kwa usalama na kutoa huduma zinazounganishwa. Hili haliwezekani ikiwa kila taasisi itaendelea kujenga mifumo na miundombinu yake kwa kujitegemea bila kuzingatia sheria, viwango na miongozo ya pamoja ya Serikali Mtandao.

Ushirikiano wa taasisi si chaguo bali ni hitaji la kimkakati. Unapunguza urudufu wa uwekezaji katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA, unaongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma na unarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mfumo wa ushirikiano, mwananchi hapaswi tena kutoa taarifa zilezile katika kila taasisi anayoihitaji badala yake, taasisi zinapaswa kuwa na uwezo wa kushirikishana taarifa kwa kuzingatia usalama, faragha na sheria zinazotumika.

Katika kufanikisha azma hiyo, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa kuweka viwango, miongozo na miundombinu ya pamoja inayowezesha taasisi kushirikiana kwa ufanisi. Jukumu hili ni msingi wa kuhakikisha uwekezaji wote wa TEHAMA serikalini unaleta thamani, unaepuka urudufu wa mifumo na unawezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Aidha, mafanikio ya Serikali Mtandao yanahitaji kila taasisi kutambua kuwa miradi ya TEHAMA si miradi ya taasisi binafsi pekee, bali ni sehemu ya mfumo mpana wa serikali. Hivyo, katika hatua za kupanga na kutekeleza miradi, taasisi zinapaswa kuzingatia usanifu wa mifumo ya serikali, matumizi ya miundombinu ya pamoja, viwango vya ubadilishanaji wa taarifa na usalama wa mifumo. Mtazamo huu unajenga mazingira ya mifumo inayoweza kuwasiliana na kubadilishana taarifa ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Kadiri mahitaji ya huduma za kidijitali yanavyozidi kuongezeka, ndivyo umuhimu wa ushirikiano unavyozidi kuwa mkubwa. Serikali Mtandao yenye mafanikio ni ile inayowawezesha wananchi kupata huduma nyingi kupitia mifumo iliyounganishwa, kwa haraka, kwa usalama na bila vikwazo visivyo vya lazima. Hii ndiyo taswira ya serikali ya kisasa inayojali muda wa wananchi na kutumia rasilimali zake kwa ufanisi.

Ni wajibu wa kila taasisi ya umma kuendelea kuimarisha ushirikiano, kuzingatia sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa ajenda ya mageuzi ya kidijitali. Ushirikiano huo utawezesha kujengwa kwa serikali inayounganishwa, inayowajibika na inayotoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Kwa pamoja, tunaweza kujenga Serikali Mtandao imara inayochochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuongeza ufanisi wa utendaji wa serikali na kuimarisha imani ya wananchi katika huduma za umma. Ushirikiano wa taasisi si msingi wa mafanikio ya Serikali Mtandao pekee, bali ni msingi wa maendeleo endelevu ya Taifa.

# Serikali yazindua

## Mifumo ya GSD na NGAO Kuimarisha Huduma za Umma




Na Benchine Bago

Serikali imezindua mifumo ya Dawati la Huduma za Serikali (Government Service Directory - GSD) na NGAO, hatua inayolenga kuimarisha utoaji wa huduma za umma kwa njia za kidijiti pamoja na kuongeza usalama wa mifumo ya Serikali.

Uzinduzi huo ulifanyika Juni 23, 2026, jijini Dodoma katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, ambapo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, alimwakilisha Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dkt. Moses Kusiluka.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Prof. Shemdoe alisema kuwa, mifumo hiyo ni sehemu ya uwekezaji wa Serikali katika kuboresha huduma kwa wananchi kupitia teknolojia.

“Mfumo wa GSD utarahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za Serikali kupitia dirisha moja, na mfumo wa NGAO utaimarisha usalama wa taarifa za Serikali kwa kutumia uthibitishaji wa vipengele vingi (Multi-Factor Authentication)”, alisema Prof. Shemdoe.

Alibainisha kuwa, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamekuwa nguzo muhimu katika kuongeza ufanisi wa Serikali kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma, kuimarisha uwazi na kupunguza gharama za utoaji wa huduma kwa wananchi.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akizindua Mifumo ya Dawati la Huduma za Serikali (Government Service Directory - GSD) na NGAO.

**"Katika dunia ya sasa matumizi ya mifumo ni jambo la lazima. Taasisi zote za umma zinapaswa kutumia mifumo ya TEHAMA kwa ufasaha ili kuboresha huduma kwa wananchi na kusimamia vizuri rasilimali watu,"** alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, aliiagiza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kuendelea kusimamia uunganishaji wa mifumo ya Serikali kupitia Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus - GovESB), ili taasisi za umma ziweze kubadilishana taarifa kwa ufanisi, kupunguza urudufu wa taarifa na kuongeza tija katika utoaji wa huduma.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi, alisema mfumo wa GSD utawarahisishia wananchi kupata huduma zote za Serikali kidijitali kupitia dirisha moja, ikiwa ni pamoja na kuona huduma zinazotolewa, gharama zake, masharti ya kupata huduma na namna ya kuzifikia hata wakiwa nyumbani kwa kutumia anwani za makazi (NAPA).

Alibainisha kuwa, zaidi ya taasisi 500 za umma tayari zimeingiza huduma zao katika mfumo wa GSD na kuzitaka taasisi ambazo bado hazijakamilisha zoezi hilo kufanya hivyo kwa wakati.

Kuhusu mfumo wa NGAO, Bw. Mkomi alisema mfumo huo ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Usalama wa Serikali Mtandao na Muongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa, Data na Mifumo ya TEHAMA Serikalini wa mwaka 2022, unaolenga kudhibiti matishio ya kimtandao yanayoweza kuathiri utendaji wa Serikali na utoaji wa huduma kwa umma.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026 yalishirikisha zaidi taasisi 226, zikiwemo Mamlaka, Mashirika ya Umma, Benki na Wizara mbalimbali ambazo zilitoa huduma na elimu mbalimbali kwa wananchi.



# Waziri Kikwete:
## Serikali Mtandao yazidi Kuimarika

**Na Catherine Peter**

Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imeendelea kuimarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA Serikalini sambamba na kuunganisha mifumo ya taasisi za umma katika mfumo jumuishi, ili kuongeza ufanisi wa Serikali katika utoaji wa huduma za umma na kuchochea upatikanaji wa huduma hizo kwa urahisi zaidi.

Hayo yameelezwa Aprili 17, 2026 Bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/27.

Waziri Kikwete alibainisha kuwa,katika kuhakikisha mifumo ya Serikali inakuwa salama wakati wote wa matumizi,e-GA imebuni na kuwezesha mfumo wa usalama wa kitaifa wa ulinzi wa mifumo ya Serikali ujulikano kwa jina la NGAO.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Ngao umeanza kutumika kwa mafanikio, ambapo taasisi na vituo vya kutolea huduma 723 tayari vimejiunga. Serikali inalenga kuhakikisha taasisi zote 780 zinazotumia mfumo wa baruapepe Serikalini (Goverment Mailing System- GMS) zinaunganishwa kwenye mfumo wa Ngao ili kuongeza usalama wa taarifa za Serikali",

alisema Mhe. Kikwete.

Aidha, tathmini ya uzingatiaji wa viwango na miongozo ya usalama wa Serikali Mtandao imefanyika katika taasisi 91 kati ya taasisi 150 zilizopangwa kufanyiwa tathmini kwa lengo la kuhakikisha kuwa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inafanya kazi kwa ufanisi, na kutoa huduma bora, salama, na endelevu kwa wananchi.

Waziri Kikwete aliliambia Bunge kwamba Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuongeza na kuboresha ufanisi kwenye miundombinu ya TEHAMA nchini ikiwemo ununuzi na uboreshaji wa seva za kuhifadhi data, kuimarisha mifumo ya umeme wa dharura, pamoja na kuboresha vituo vya kuhifadhi taarifa.

“Pia Serikali kupitia e-GA ilifanya uhuishaji wa miundombinu ya vituo vya kuhifadhi data na taarifa kwa kununua vifaa vya TEHAMA, kuboresha mfumo wa umeme wa dharura (power backup), kununua vifaa vya miundombinu ya kangavuke (generator) kwa ajili ya kuwezesha mifumo ya kiotomatiki kufanya kazi”, alifafanua Mhe. Kikwete .

Kadhalika Waziri Kikwete alisema kuwa, Serikali kupitia e-GA imeendelea kupanua huduma za Serikali Mtandao kwa kuunganisha mifumo mbalimbali kupitia Mfumo



Usalama wa Mifumo Umeimarishwa

wa Pamoja wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (GovESB), ambapo hadi kufikia Machi 2026 jumla ya mifumo 252 kutoka taasisi 200 imeunganishwa .

Mifumo hiyo inahusisha sekta muhimu ikiwemo Mahakama, Polisi, TAKUKURU na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambazo zimewezeshwa na mfumo kuwasiliana na kubadilishana taarifa ili kurahisisha utendaji kazi wa kila siku.

**“Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa upande mwingine, juhudi zimefanyika katika kuunganisha taasisi 660 kwenye mtandao wa mawasiliano wa Serikali (Government Network), pamoja na kuanzisha na kuboresha mifumo mbalimbali ikiwemo e-Office, e-Mrejesho, e-Ukaguzi na e-Mikutano ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi.”** Alisema Waziri Kikwete.


Pamoja na hayo,Waziri Kikwete pia aliliambia Bunge kuhusu mafanikio mbalimbali ambayo Serikali imeyapata ndani na nje ya nchi katika utekelezaji wa afua za Serikali Mtandao.

Kikwete, alibainisha kuwa Tanzania imepata kutambuliwa kimataifa kufuatia ubunifu na matumizi madhubuti ya mifumo ya Serikali Mtandao.

Alieleza kuwa mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (e-Mrejesho v2) umeiwezesha nchi kushinda tuzo ya World Summit on the Information Society 2025 (WSIS Grand Champion), tuzo inayotolewa kwa miradi bunifu ya TEHAMA duniani.

Mbali na mafanikio hayo, Waziri Kikwete alibainisha kuwa Tanzania imeorodheshwa katika Kundi A la nchi zenye ukomavu wa juu wa matumizi ya teknolojia serikalini (Extensive GovTech Maturity), kwa mujibu wa tathmini ya Benki ya Dunia.

**“Mheshimiwa Mwenyekiti,mafanikio haya yanaonesha juhudi za Serikali katika kuimarisha huduma za kidijitali na ushirikishwaji wa wananchi.Kwa ujumla, mafanikio haya yanaonesha dhamira ya Serikali ya Tanzania ya kujenga mfumo imara wa Serikali Mtandao unayolenga kutoa huduma bora, salama na za haraka kwa wananchi.”** Alifafanua Waziri Kikwete.



# Kujituma, Uadilifu na Weledi vyamletea Bi. Khadija Mzenzi Tuzo ya Mfanyakazi Bora e-GA 2025/2026

"Kupitia utendaji kazi wake mzuri, Menejimenti iliona anastahili kuwa mshindi kwani amechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha utoaji wa huduma za Mamlaka na kufanikisha malengo ya taasisi".



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais UTUMISHI Bw. Juma Mkomi wakisikiliza maelezo ya Huduma za e-GA kutoka kwa Bi. Khadija Mzenzi walipotembelea banda la e-GA kwenye maoesho ya wiki ya Utumishi wa Umma 2025 Jijini Dodoma

**Na Queenter Mawinda**

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imemtangaza Afisa TEHAMA, Bi. Khadija Mzenzi, kuwa Mfanyakazi Bora wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa kutambua utendaji wake uliotukuka, unaoambatana na kujituma, uadilifu na weledi katika kutekeleza majukumu yake. Tuzo hiyo pia inadhihirisha nafasi yake kama mfano wa kuigwa kwa watumishi wenzake katika kuendeleza utamaduni wa uwajibikaji, ubora na utoaji wa huduma bora.

Bi. Khadija aliibuka mshindi katika uchaguzi wa mfanyakazi bora wa Mamlaka uliofanyika April 27 mwaka huu, baada ya kushindanishwa wafanyakazi bora 18 kutoka katika Idara na Vitengo, na kisha Menejimenti kupiga kura ili kumpata mfanyakazi bora wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Meneja Rasilimaliwatu na Utawala wa Mamlaka Bw. Jafari Maganga alisema, Mamlaka ilifanya uchaguzi wa ndani kwa kila Idara na Vitengo ili kupata mfanyakazi bora na kisha orodha hiyo iliwasilishwa Menejimenti kwa ajili ya kumchagua mfanyakazi bora wa taasisi.

Alisema, Menejimenti iliwapima watumishi wote bora waliochaguliwa kutoka kwenye Idara na Vitengo na kisha kupiga kura kwa uwazi ili kumchagua mfanyakazi bora wa Mamlaka, kwa kuzingatia vigezo vilivyopo bila upendeleo wa aina yeyote.

**"Uchaguzi huo ulifanyika kwa kupiga kura ya wazi na kuwapata washindi watatu walioingia tatu bora na hatimaye kumpata mfanyakazi bora wa jumla wa Taasisi",** alisisitiza Bw. Jafari.

Aidha, Bw. Maganga alisema Bi. Mzenzi amekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na wenzake kutoa suluhisho bunifu na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ili kuongeza tija katika utendaji wa kazi. Pia, amewahi kushiriki kutoa mafunzo ya mifumo ya TEHAMA kwa taasisi mbalimbali za umma, jambo linaloonesha utaalamu na mchango wake katika kuimarisha huduma za kidijitali serikalini.

Alisema kutambuliwa kwake kama mfanyakazi bora ni ishara ya kuthamini juhudi, nidhamu na uwajibikaji wake, na kutoa morali kwa watumishi wengine kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo.

Naye Bi. Khadija, ametoa shukrani zake kwa watumishi na menejimenti ya Mamlaka kwa kutambua juhudi na utendaji kazi wake, uliopelekea kuchagulia kupata ushindi huo. Aliahidi kuendelea kuwa mfano bora kwa watumishi wenzake katika uzingatiaji wa maadili ya utumishi wa umma, pamoja na kufanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha Mamlaka inafikia malengo yake.



# Naibu Waziri - UTUMISHI Ahamasisha Ubunifu wa Teknolojia zinazochipukia Kuboresha Huduma za Serikali

**Na Benchine Bago**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Ndege Qwaray (Mb), amefanya ziara ya kikazi katika Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (Research, Innovation and Development Centre – RIDC) kilichopo jijini Dodoma, ambapo amekagua miradi mbalimbali ya TEHAMA inayotekelezwa na kituo hicho kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma Serikalini.

Katika ziara hiyo iliyofanyika Mei 18, mwaka huu, Mhe. Qwaray alipata fursa ya kutembelea na kujionea miradi ya kiteknolojia inayolenga kutoa suluhisho kwa changamoto katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya na utawala. Aidha, miradi hiyo inahusisha matumizi ya teknolojia zinazochipukia kama vile Internet of Things (IoT) na Akili Mnemba (AI), katika kurahisisha utendaji kazi Serikalini na kuongeza ufanisi wa huduma kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mhe. Qwaray ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa juhudi zake za kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana, kupitia tafiti na ubunifu wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA yenye mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa.

"Niwapongeze e-GA kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kukuza ubunifu na tafiti za teknolojia. Dunia ya sasa inabadilika kwa kasi kubwa kutokana na maendeleo ya teknolojia, hivyo ni muhimu kuendelea kujifunza, kufanya tafiti na kubuni mifumo mipya itakayokwenda sambamba na mabadiliko hayo." Amesema Mhe. Qwaray.

Amesisitiza kuwa, bunifu zote zinazotengenezwa zinapaswa kuwa na tija kwa jamii na kuchangia moja kwa moja katika kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi pamoja na kuongeza ufanisi ndani ya taasisi za Serikali.

Sambamba na hilo, Mhe. Qwaray amesisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano kati ya e-GA, vyuo vikuu na sekta binafsi ili kuongeza uwekezaji katika tafiti, ubunifu



na maendeleo ya teknolojia zinazoweza kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, amesema kituo hicho kimeendelea kuwa chachu ya mageuzi ya kidijitali Serikalini kupitia ujenzi wa mifumo mbalimbali inayotumika katika taasisi za umma.

Ametaja baadhi ya mifumo hiyo kuwa ni Mfumo wa Uendeshaji wa Vikao vya Bodi na Menejimenti (e-Board) pamoja na Mfumo wa Uendeshaji wa Vikao Kidijitali (e-Mikutano), ambayo imekuwa ikisaidia kuongeza ufanisi katika shughuli za Serikali.

**“Kituo hiki kimekuwa na manufaa makubwa kwa taifa kutokana na kazi zake za utafiti, ubunifu na maendeleo ya mifumo ya TEHAMA. Pia, kimefungua fursa kwa wanafunzi na vijana wenye taaluma ya TEHAMA kushiriki katika tafiti na bunifu mbalimbali kwa maslahi ya taifa.”** Amefafanua Mha. Ndomba.

Katika kuonesha dhamira ya Serikali kuendelea kuimarisha kituo hicho, Mhe. Qwaray ameahidi kuwa Wizara itaendelea kushirikiana na e-GA kutatua changamoto zinazoikabili RIDC ili kuongeza fursa kwa vijana wengi zaidi wa Kitanzania kupata nafasi ya kujifunza, kufanya tafiti na kushiriki katika ubunifu wa teknolojia mbalimbali za kisasa.






# Mhe. Ridhiwani

## Aipongeza e-GA Ujenzi wa Mifumo Bunifu

**"Ninajivunia sana kila ninapotembelea maonesho na kukuta e-GA ikiwa imeleta suluhisho la changamoto mbalimbali kupitia mifumo ya kidijitali inayosaidia kuboresha utendaji wa taasisi za Serikali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma."**

Mhe. Ridhiwani Kikwete - Waziri ORMUUUB



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), akisikiliza maelezo ya huduma mbalimbali za Serikali Mtandao kutoka kwa Afisa Habari Mwandamizi Bi. Catherine Peter wakati alipotembelea banda la e-GA kwenye Mkutano wa Pili wa Jumuiya za Wataalamu wa Utawala na Rasilimaliwatu (AAPAM) Jijini Arusha

**Na Catherine Peter**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa juhudi zake za kuendelea kujenga Serikali kidijitali kupitia mifumo mbalimbali inayorahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza ufanisi katika taasisi za umma.

Mhe. Ridhiwani ametoa pongezi hizo alipofungua Mkutano wa Pili wa Jumuiya za Wataalamu wa Utawala na Rasilimaliwatu (AAPAM) Tawi la Tanzania na kutembelea banda la maonesho la e-GA, lililopo jijini Arusha Mei 6, 2026.

Aidha, amesisitiza kuwa ni wajibu wa kila taasisi ya Serikali kutumia kikamilifu mifumo ya kielektroniki ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa wakati, kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake, Afisa TEHAMA kutoka e-GA, Bi. Khadija Mzenzi, akimwelezea Waziri huyo kuhusu mfumo wa e-Barua, amesema mfumo huo umebuniwa na kusanifiwa na e-GA kwa lengo la kutatua changamoto ya watumishi kushindwa kusoma au kushughulikia baruapepe wanapokuwa katika maeneo yasiyo na huduma ya intaneti.

Bi. Mzenzi amesema mfumo huo unamwezesha mtumiaji kufungua na kusoma baruapepe ambazo tayari alishazipokea na kuzifungua awali hata akiwa nje ya mtandao, jambo linalorahisisha ufuatiliaji wa mawasiliano ya kikazi na kupunguza ucheleweshaji wa huduma kwa wananchi.

Ameongeza kuwa mfumo wa e-Barua pia unaruhusu mtumiaji kuandaa na kutuma baruapepe akiwa katika mazingira yasiyo na mtandao. Ujumbe huo huhifadhiwa kwenye kifaa husika na kutumwa moja kwa moja pindi kifaa kinapopata huduma ya intaneti.

Akifafanua zaidi kuhusu usalama wa mfumo huo, Bi. Mzenzi amesema kuwa mtumishi anayetumia e-Barua anatakiwa kuwa na kifaa kinachoruhusu matumizi ya teknolojia za alama za kibayometriki, ikiwemo utambuzi wa alama za vidole na sura, ili kuimarisha ulinzi na usalama wa taarifa za mtumiaji.

Mfumo wa e-Barua ni miongoni mwa ubunifu wa kidijitali unaoendelezwa na e-GA kwa lengo la kuboresha mawasiliano ya Serikali, kuongeza tija kwa watumishi wa umma na kuharakisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.




# Epuka Dawa za Miujiza, Chagua Njia Salama ya Kupunguza Uzito

**Na Queenter Mawinda**

Kuongezeka kwa uzito miongoni mwa wafanyakazi, kumeendelea kuwa changamoto inayochangiwa na mtindo wa maisha unaohusisha kukaa muda mrefu kwenye dawati, kufanya shughuli zinazohitaji matumizi madogo ya nguvu za mwili na ulaji usiozingatia lishe bora.

Wafanyakazi wengi huanza siku kwa kifungua kinywa, hula chakula cha mchana wakiwa ofisini na kumalizia kwa chakula kingi usiku baada ya kazi, huku wengi wakikosa muda wa kufanya mazoezi ya mwili. Wataalamu wa afya wanatoa onya juu ya mtindo huu wa maisha kuwa unaongeza hatari ya kupata uzito uliopitiliza na hivyo kuongeza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, shinikizo la damu na magonjwa ya moyo.

Afisa Lishe na Muuguzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dkt. Zainabu Tindi, anasema sababu kuu zinazochangia ongezeko la uzito ni mfumo bwete wa maisha unaokosa shughuli za mwili na kula chakula kupita kiasi bila kuzingatia mlo kamili.

Anasema watu wanaofanya kazi za ofisini wanapaswa kuwa makini zaidi na uchaguzi wa vyakula wanavyokula, kiasi cha chakula wanachotumia na kuhakikisha wanapata muda wa kufanya mazoezi angalau dakika 30 hadi 45 kila siku.



Afisa Lishe na Muuguzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dkt. Zainabu Tindi (kulia), akifanya mahojiano na Afisa Habari Mwandamizi wa e-GA, Bi. Queenter Mawinda kuhusu lishe Bora hasa katika kupunguza uzito kupitia njia salama ya lishe

Dkt. Tindi anasema lishe bora inahusisha kupunguza vyakula vya wanga huku mboga za majani zikipewa nafasi kubwa kwenye sahani ya chakula. Lakini pia, mazoezi ya kutembea ni salama na yenye manufaa kwa watu wenye uzito mkubwa kuliko kuanza mazoezi ya kukimbia.

**"Mtu anayetaka kupunguza uzito anapaswa kuhakikisha mboga za majani zinachukua takribani asilimia 50 ya chakula anachokula. Aidha, ale matunda kwa kiasi kinachofaa, atumie nafaka ambazo hazijakobolewa na kupendelea vyakula vilivyopikwa kwa mvuke,"** anasema Dkt. Tindi.

Alisisitiza pia umuhimu wa kupunguza matumizi ya mafuta na vyakula vyenye sukari nyingi pamoja na kupunguza ulaji wa wanga taratibu badala ya kuacha ghafla.

## Kuruka mlo si suluhisho la kudumu

Kuhusu tabia ya kuruka milo ili kupunguza uzito, Dkt. Tindi anasema inaweza kusaidia katika mazingira fulani, lakini haipaswi kufanywa bila mwongozo wa kitaalamu. Anashauri kula mapema jioni, ikiwezekana kabla ya saa 12 jioni, huku chakula cha usiku kikizingatia mbogamboga nyingi na kupunguza au kuacha wanga.

Anasisitiza kuwa unywaji wa maji ni sehemu muhimu ya mpango wa kupunguza uzito. Mtu anashauriwa kunywa angalau glasi nane (8) za maji au takribani lita moja na nusu kwa siku, kutegemeana na hali ya hewa na aina ya kazi anayofanya.

## Njia salama za kupunguza uzito

Kwa mujibu wa Dkt. Tindi, kabla ya kuanza mpango wa kupunguza uzito ni muhimu kufanya tathmini ya afya kwa kupima uzito, urefu na mzunguko wa kiuno. Kwa wanawake, mzunguko wa kiuno usizidi sentimita 88, huku kwa wanaume usizidi sentimita 102.

Pia anashauri kupima shinikizo la damu, kiwango cha sukari kwenye damu, cholesterol pamoja na afya ya ini na figo.

Mbali na lishe bora, anashauri watu:

- Kuchagua nafaka zisizokobolewa.
- Kula mboga za majani na matunda kwa wingi.
- Kunywa maji badala ya vinywaji vya sukari kama soda na juisi
- Kupata usingizi wa saa 7 hadi 9 kwa siku.
- Kupunguza msongo wa mawazo.
- Kufanya mazoezi ya kutembea kwa dakika 30 hadi 45 kila siku. Kwa watu wenye uzito mkubwa, kutembea ni salama zaidi kuliko kukimbia.

**Matokeo huonekana taratibu**

Dkt. Tindi anasema matokeo ya kupungua uzito hutofautiana kati ya mtu na mtu. Wengine wanaweza kuona mabadiliko ndani ya miezi miwili (2), huku wengine wakihitaji hadi miezi sita (6) kulingana na hali yao ya kiafya na namna wanavyofuata ushauri wa lishe. Lakini kiafya hushauriwa mtu kupungua nusu kilo ½ hadi kilo 4 kwa mwezi.

## Tahadhari dhidi ya dawa za kupunguza uzito

Anawaonya wananchi dhidi ya matumizi ya dawa au virutubisho vinavyouzwa mitandaoni kwa madai ya kupunguza uzito haraka.

"Dawa nyingi zinazouzwa bila usimamizi wa kitaalamu zinaweza kuwa na madhara makubwa. Mtu anaweza kupoteza madini muhimu mwilini au kupata matatizo mengine ya afya. Tunashauri watu watumie njia za asili na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya," Alisisitiza Dkt. Tindi

## Changamoto na makosa yanayofanywa na wengi

Kwa mujibu wa Dkt. Tindi, changamoto kubwa kwa watu wanaotaka kupunguza uzito ni kukosa ushauri sahihi kutoka kwa wataalamu. Wengine hupata kushuka kwa kiwango cha sukari mwilini, kuona hafifu au ngozi kupoteza afya kutokana na mbinu zisizo sahihi.

Anataja makosa mengine kuwa ni kutokufanya mazoezi, kunywa vinywaji vyenye sukari nyingi, kula usiku sana na kupunguza wanga kwa ghafla badala ya kufanya hivyo hatua kwa hatua.

## Kudumisha uzito uliopungua

Dkt. Tindi anasema changamoto kubwa kwa watu wengi si kupunguza uzito, bali ni kuendelea kuudhibiti baada ya kufikia lengo. Watu wengi hurejea kwenye mtindo wao wa zamani wa maisha kwa kuacha mazoezi, kuongeza ulaji wa vyakula vyenye wanga na mafuta mengi au kula bila mpangilio, jambo linalosababisha uzito kurejea kwa haraka.

Anasema siri ya kudumisha uzito uliopungua ni kuifanya lishe bora kuwa sehemu ya maisha ya kila siku badala ya mpango au kampeni ya muda mfupi.



Dkt. Zainabu Tindi

**“Mabadiliko huanzia kwenye fikra. Mtu akiamua kuishi maisha yenye lishe bora na mazoezi, ana nafasi kubwa ya kudumisha uzito wake kwa muda mrefu,”** anasema.

**Lishe hutofautiana kulingana na umri**

Dkt. Tindi anaeleza kuwa mahitaji ya lishe hutegemea umri.

- Watoto wanahitaji protini nyingi, madini kama calcium kwa ukuaji wa mifupa, vitamini A pamoja na mafuta yenye Omega-3 kwa maendeleo ya ubongo.
- Vijana wanahitaji mlo kamili unaosaidia ukuaji wa mwili, huku watu wazima wakishauriwa kula mboga nyingi za majani, samaki, dagaa, nyama nyeupe, maziwa ya mtindi, karanga, korosho, mayai, parachichi kwa kiasi na vyakula vinavyosaidia afya ya mifupa.
- Ushauri kwa jamii

Dkt. Tindi anasisitiza kuwa mtu anayehitaji kupunguza uzito anapaswa kufika hospitalini kwa ajili ya kupimwa uzito, urefu na kupata mpango maalumu wa lishe unaoendana na mahitaji yake.

Aidha, alizitaka taasisi za afya kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu lishe bora na udhibiti wa uzito ili kupunguza ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza na kusisitiza kuwa lishe bora, mazoezi ya mara kwa mara, usingizi wa kutosha na afya nzuri ya akili ndiyo nguzo muhimu za kupunguza uzito kwa njia salama na kudumisha afya kwa muda mrefu.



Baadhi ya Vyakula vinavyochangia ongezeko la uzito wa mwili.





# TEHAMA

## Ilivyobadili Maisha ya Joseph kutoka Utegemezi hadi Ubunifu

Na Benchine Bago

Safari ya Joseph Joakimu Mtei, ni ushahidi kwamba teknolojia inaweza kuwa daraja la kuvuka vikwazo vinavyoonekana kuwa vigumu. Kupitia TEHAMA, ameweza kujijengea taaluma, kujitegemea kiuchumi na kuwa chachu ya matumaini kwa vijana wengi wenye ulemavu.


Simulizi yake inakumbusha kuwa uwezo wa binadamu haupimwi kwa viungo alivyokosa, bali kwa uthubutu wa kutumia alichonacho kutimiza ndoto zake. Joseph ameigeuza miguu yake kuwa chombo cha ubunifu na mafanikio, akithibitisha kuwa fursa, elimu na teknolojia vinapounganishwa, vinaweza kubadili maisha na kufungua milango ya mustakabali wenye matumaini kwa kila mmoja.

Hii ilionekana katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026, ambapo Mamlaka ya Ufundi Stadi VETA, ilikuwa ni miongoni mwa taasisi za umma zilizoshiriki maonesho hayo, ambapo kijana Joseph alikuwa ni miongoni mwa watumishi wa VETA, waliotoa elimu na huduma mbalimbali za taasisi hiyo.

Wengi wetu tumezoea kutumia mikono tunapofanya kazi kwa kutumia kompyuta. Hata hivyo, hali ni tofauti kwa Joseph, ambaye ni mlemavu asiye na mikono. Licha ya changamoto hiyo, ametafuta mbinu mbadala na hutumia miguu yake kuendesha kompyuta na kutekeleza majukumu mbalimbali kwa ufanisi. Uwezo wake unaonyesha kuwa ulemavu si kikwazo cha kufikia malengo pale panapokuwapo dhamira, ubunifu na ustahimilivu.

Miguu?! Ndiyo. Miguu ndiyo inayofanya kazi. Tena si kazi ya kawaida, bali kazi zinazogusa maisha ya watu na kuleta mabadiliko makubwa katika enzi hizi za maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Mawasiliano.

Kwa wengi, kutumia kompyuta kunamaanisha kutumia mikono. Lakini kwa Joseph Joakimu Mtei, miguu ndiyo zana yake kuu ya kazi. Kwa ustadi wa hali ya juu, hutumia miguu yake kuendesha kompyuta na kubuni samani pamoja na kuchora ramani za majengo (Civil Drafting), akithibitisha kwamba



Bw. Joseph Joakimu Mtei, akionesha namna anavyoweza kusanifu michoro mbalimbali katika kompyuta kwa kutumia miguu yake.

uwezo wa mtu haupimwi na ulemavu wake, bali na dhamira, maarifa na bidii aliyonayo.

Joseph, kijana mwenye umri wa miaka 25, mzaliwa wa Rombo mkoani Kilimanjaro, anaandika historia yake upya kupitia matumizi ya TEHAMA. Ingawa alizaliwa bila mikono, hakuruhusu hali hiyo kuwa kikwazo cha kutimiza ndoto zake. Badala yake, ameigeuza changamoto hiyo kuwa chanzo cha ubunifu, uthubutu na mafanikio yanayowahamasisha wengi ndani na nje ya Tanzania.

“Kikubwa ni kujikubali na hali uliyonayo na kutafuta namna bora ya kukabiliana na changamoto za maisha kwa vile ambavyo Mungu amekuumba.” anaeleza huku akiwa na tabasamu pana linalosadifu kile ambacho anakiongea, kujikubali!

Kwa miaka mingi, jamii ilimuona kama mtu wa kuhurumiwa. Lakini Joseph aliona kitu tofauti: fursa ya kufikiri nje ya boksi ili kupata njia ya kuelekea kwenye kujitegemea kutoka utegemezi.

**“Nilianza kujifunza kompyuta nilipokuwa shule ya msingi pale St.Fransic (St Francis of Assisi Primary School) iliyopo Bomang’ombe Wilayani Hai, katika mkoa wa Kilimanjaro. Walimu walinifundisha kuumba herufi, lakini mimi nikaanza kujifunza mwenyewe kuchora kwa kutumia kompyuta”,** anaeleza.

Kila kitu kilibadilika kwa Joseph baada ya kugundua kwamba kupitia TEHAMA anaweza kubadilisha maisha yake na ulimwengu mpya ulifunguka. Kwa sasa Joseph amepata ajira ya muda ya msaidizi wa karakana (workershop assistant) katika kampuni ya Ujuzi Incorporated Co. Ltd ambayo ni kampuni tanzu ya VETA, huku akiendelea na masomo yake katika ngazi ya diploma ya ufundi stadi.

Hapo awali, kabla ya kujiunga na masomo VETA, Joseph alitumia uwezo wake katika TEHAMA kufanya kazi ya kuhamisha nyimbo kutoka kwenye kompyuta na kuweka kwenye simu ili apate kipato cha kujikimu.

**“Baada ya kupata pesa kidogo nilinunua kompyuta yangu ya kwanza ambayo ilinisaidia kujifunza mambo mbalimbali, kupitia kazi yangu nayoifanya nimeweza kujitegemea na kumsomesha mdogo wangu hapahapa VETA ili naye apate ujuzii”**, anafafanua.

Hata hivyo, Joseph anabainisha kuwa, changamoto kubwa inayomkabili kwa sasa ni fedha ya kupata



Bw. Joseph Joakimu Mtei, akionesha namna anavyoweza kusanifu michoro mbalimbali katika kompyuta kwa kutumia miguu yake.

kompyuta yenye ufanisi mkubwa kulingana na mahitaji ya kiteknolojia. “Nahitaji kompyuta yenye uwezo mkubwa, na aina hiyo ya kompyuta ni gharama sana,hivyo naendelea kujitafuta ili niweze kuipata .” anasisitiza.


Kaimu Meneja Ujuzi wa Incorporated Co. Ltd Mhandisi Marco Kapinga, ndiyo aliyegundua uwezo wa Joseph katika eneo la ubunifu katika maadhimisho ya miaka 30 ya VETA.

“Nilipomuona akitumia miguu kuchora samani na ramani, nilijua kijana huyu ana uwezo wa ziada,” anasema Mhandisi Kapinga na kubainisha kwamba, bidhaa nyingi ambazo Joseph alibuni zilipendwa sokoni.


**“Nilimuona ana uwezo mkubwa katika eneo la ubunifu kwa kutumia TEHAMA, hivyo niliona ni mtu sahihi kwenye karakana yetu, baada ya kumuingiza kwenye timu yetu na kumpa majukumu mbalimbali tulimjengea uwezo kwenye matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwemo software za ‘Autocard’”**, anasema Kapinga.

Mhandisi Kapinga anaeleza kwamba, Joseph ana uwezo na kasi kubwa katika kutimiza majukumu na huwezi kuona tofauti ya bunifu iliyotengenezwa na Joseph kwa mguu mmoja na ile iliyobuniwa na kijana mwenye mikono miwili.

Hadithi hii murua ya Joseph inafundisha jambo moja: ulemavu wa viungo si ulemavu wa akili. TEHAMA imevunja kuta nne zilizokuwa zikitenga vijana wenye ulemavu na fursa, hivyo vijana wakiitumia vema TEHAMA huwasaidia kujikwamua kiuchumi.




Bw. Joseph Joakimu Mtei




# e-Ardhi : Mageuzi ya Kidijiti yanavyosogeza Huduma za Ardhi Karibu na Wananchi

**Na. Eleuteri Mangi | Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Kadiri Tanzania inavyoendelea kujenga uchumi wa kidijiti, ndivyo huduma za umma zinavyozidi kusogezwa karibu na wananchi. Leo, mwananchi anaweza kupata huduma mbalimbali kwa haraka na kwa uwazi zaidi kupitia mifumo ya kidijiti inayounganisha wananchi na taasisi za serikali.

Katika sekta ya ardhi, mageuzi hayo yamejidhihirisha kupitia Mfumo wa kisasa wa e- Ardhi ulioanzishwa na Serikali kwa lengo la kurahisisha huduma za ardhi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa wakati, haraka, uwazi na ufanisi zaidi.

Katika dunia ya sasa ambayo ina kasi kubwa ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutekeleza mageuzi makubwa ya kidijiti yanayoboresha utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi.

Mfumo wa e-Ardhi umeanzishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili wananchi wapate huduma za upangaji, upimaji, umilikishaji wa ardhi, usajili wa hati, usajili wa nyaraka za kisheria pamoja na huduma za uthamini kwa njia ya kidijiti popote walipo.

Kupitia mfumo huo, wananchi hawalazimiki tena kutumia muda na gharama kubwa kufuatilia huduma kutoka ofisi moja hadi nyingine, kwani huduma nyingi sasa zinapatikana kwa urahisi zaidi kupitia mfumo huo wa kielektroniki.

Akiwasilisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2026/27 Mei 28, 2026 Bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Leonard Akwilapo, alieleza kuwa serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za ardhi ili kuongeza ufanisi, uwazi na kurahisisha upatikanaji

wa huduma za ardhi kwa wananchi.

Dhamira hiyo inaendana na maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyesisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa ardhi unaochochea maendeleo endelevu ya taifa wakati wa uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la 2023 pamoja na Mfumo wa e-Ardhi uliofanyika Dodoma Machi 17, 2025.

Jambo la kujivunia zaidi, mfumo wa e-Ardhi umesanifiwa na kujengwa na wataalamu wa ndani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Hii ni uthibitisho kuwa Tanzania ina wataalamu wenye uwezo wa kutengeneza mifumo ya kisasa inayokidhi mahitaji ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mbali na kurahisisha utoaji wa huduma, mfumo wa e-Ardhi umeongeza usalama wa nyaraka za ardhi kwa kuweka alama maalum za uthibitishaji (Barcode) zinazomwezesha mwananchi kuhakiki uhalali wa nyaraka alizopewa. Hatua hii imeongeza uaminifu wa huduma na kupunguza uwezekano wa udanganyifu.

Faida za mfumo huu zimeanza kuonekana kwa wananchi wengi wanaonufaika na huduma zake katika maeneo mbalimbali nchini. Wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka



**Bw. Eleuteri Mangi**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

2026 ambayo yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma, baadhi ya wananchi walieleza namna mfumo huo ulivyowasaidia kupata huduma kwa haraka na kwa urahisi zaidi ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali.

Bi. Latifa Njogoro kutoka Mkoa wa Dodoma anashuhudia kuwa mfumo wa e-Ardhi umemrahisishia mchakato wa kupata hati ya ardhi yake kwa muda mfupi zaidi akisema mfumo umemwezesha kufuatilia hatua za maombi yake kwa urahisi na kupata taarifa kwa wakati bila usumbufu wowote.

Ushuhuda huo ni kielelezo cha namna teknolojia na hasa mfumo wa e-Ardhi unavyoendelea kuboresha maisha ya wananchi na kuimarisha utoaji wa huduma za sekta ya ardhi nchini.

Sasa ni muda muafaka wananchi kuendelea kutumia mfumo wa e-Ardhi na kuamini huduma zinazotolewa ambapo matumizi ya mfumo huo siyo tu yanaokoa muda na gharama, bali pia yanachangia kujenga mfumo wa kisasa wa usimamizi wa ardhi wenye uwazi, usalama, ufanisi mkubwa na kukusanya mapato ya serikali.

Kwa kuzingatia mafanikio yanayoendelea kupatikana kupitia mfumo wa e-Ardhi, mfumo huo si tu umeongeza ufanisi, uwazi na usalama wa huduma, bali pia umeonesha uwezo mkubwa wa wataalamu wa ndani katika kubuni na kuleta nchini suluhisho la kidijiti katika sekta ya ardhi linalokidhi mahitaji ya Watanzania.

Hivyo, wananchi wanahimizwa kuendelea kutumia mfumo wa e-Ardhi ili kunufaika na huduma za haraka, salama na zinazopatikana kwa urahisi zaidi. Kadiri matumizi ya mfumo huo yanavyoendelea kuongezeka, ndivyo sekta ya ardhi inavyozidi kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Hakika, kupitia e-Ardhi, Serikali inaendelea kutekeleza kwa vitendo falsafa ya **"Kazi na Utu, Tunasonga Mbele"** kwa kuhakikisha huduma bora zinawafikia wananchi kwa wakati, kwa uwazi na kwa heshima inayostahili. Haya ni mageuzi yanayomgusa mwananchi moja kwa moja na kuifanya Tanzania kusonga mbele katika safari ya kujenga taifa la kidijiti lenye maendeleo jumuishi na endelevu.

# Maonesho



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb), akisikiliza maelezo ya huduma mbalimbali za Serikali Mtandao kutoka kwa Meneja Mawasiliano wa e-GA Bi. Subira Kaswaga wakati alipotembelea banda la e-GA kwenye Mkutano wa Pili wa Jumuiya za Wataalamu wa Utawala na Rasilimaliwatu (AAPAM) Jijini Arusha.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Dkt. Charles Msonde (kushoto) akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mhandisi Benedict Ndomba, wakati alipotembelea banda la maonesho la Mamlaka wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Jijini Dodoma

# Uzinduzi wa Mifumo



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akizungumza wakati wa kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Jijini DOdoma.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.

# Zawadi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi Cheti Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bi. Ndili Yusuph, kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa GSD.

# Zawadi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bw. Noel Mwadende, kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bw. Sebastian Mvungi kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.

# Zawadi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Afisa TEHAMA Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bw. Denis Bahati kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) Mhe. Prof. Riziki Shemdoe akimkabidhi tuzo Afisa TEHAMA wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Bw. Nenge Masoya kwa kutambua mchango wake katika utengenezaji wa Mfumo wa Ngao.

# Kikao cha Baraza



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mhandisi Benedict Ndomba akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Serikali Mtandao wakati wa Kikao cha baraza Jijini Dar Es Salaam.



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Serikali Mtandao wakijadili masuala mbalimbali yanayohusu Mamlaka wakati wa Kikao cha baraza Jijini Dar Es Salaam.

Ofisi ya Rais,
Mamlaka ya Serikali Mtandao,
Mtaa wa Mawasiliano,
S.L.P 2833,
40404 DODOMA.

**Baruapepe:** barua@ega.go.tz
**Tovuti:** www.ega.go.tz